

chanjo ya UVIKO-19 kwa ujauzito



Chanjo ya UVIKO-19 inapendekezwa wakati wa ujauzito.

Chanjo ndiyo njia bora zaidi ya kujikinga wewe na mtoto wako ambaye hajazaliwa kutokana na hatari zinazojulikana za UVIKO-19 wakati wa ujauzito.



Hatari za UVIKO-19 wakati wa ujauzito kwako na kwa mtoto




Wagonjwa wa UVIKO-19 ambao ni wajawazito wana uwezekano mkubwa wa kudhoofika sana na kuitaji uangalizi wa karibu hospitalini.

- > Kuzaliwa kabla ya wakati na kuzaa mtoto aliyekufa ni kawaida zaidi ikiwa utapatwa na UVIKO-19 ukiwa mjamzito.
- > Baadhi ya ushahidi wa maambukizi ya UVIKO-19 wakati wa ujauzito huongeza hatari ya kuharibika kwa mimba.



Chanjo za UVIKO-19 ni salama wakati wa ujauzito



Chanjo za UVIKO-19 hazina viambata vinavyojulikana kuwa hatari kwa wajawazito au kwa mtoto anayekua. Viungo havivuki kwenye plasenta au kumfikia mtoto.

- > Chanjo ya UVIKO-19 **hupunguza** kiwango cha vifo vya watoto kabla ya kuzaliwa.
- > Chanjo za UVIKO-19 **haziwezi** kukupa wewe au mtoto wako ugonjwa wa UVIKO-19.
- > Chanjo kwa wajazito inahusishwa na **KUPUNGUZA** ongezeko la hatari ya:
 - × Mimba kuharibika
 - × Kuzaliwa kabla ya wakati
 - × kifo ch mtoto kabla ya kuzaliwa
 - × Matatizo wakati wa kujifungua
 - × kujifungua mtoto mwenye matatizo
 - × Mtoto kuzaliwa mdogo kuliko ilivyotarajiwa
 - × Mtoto kuwa na matatizo ya afya katika miezi sita ya kwanza ya maisha



Chanjo za COVID-19 zinafaa kwa ujauzito



Nzuri sana katika kulinda dhidi ya ugonjwa wa wastani na mbaya wa UVIKO-19.

- > Chanjo wakati wa ujauzito humpa mtoto wako kinga dhidi ya UVIKO-19 mara tu wanapozaliwa.

Ushahidi kutoka tafiti **38**, katika **nchi 10**, ikiwa ni pamoja na **watu 367,746** waliochanjwa au walioongezewa chanjo wakiwa ujauzito

Hatua zote za ujauzito ni sababu ya hatari kwa UVIKO-19. Ikiwa una mjamzito wakati wa msimu wa chanjo, utapewa chanjo ya nyongeza ya UVIKO-19.

